**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**652** **ELIMU KWA MICHEZO**

**Muda: Saa 3.** **Mwaka : 2014**

---

**MAELEKEZO.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C** yenye jumla ya maswali **kumi na sita (16)**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka kila sehemu **B** and **C**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na sehemu **B** na **C** zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Vikokotozi **haviruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (40 Alama)

Jibu maswali yote katika sehemu hii

1. Eleza maana ya rasilimali vitu katika michezo na umuhimu wake.
2. Taja michezo minne ya asili inayochezwa na watoto na eleza mchango wake katika kujenga umoja.
3. Fafanua hatua nne za kufuata wakati wa kudaka mpira katika mchezo wa kikapu.
4. Bainisha sheria nne zinazotakiwa kuzingatiwa katika mchezo wa tenisi.
5. Eleza stadi nne muhimu za msingi katika mpira wa netiboli.
6. Eleza faida nne zinazopatikana kwa kijiji kinapoandaa mashindano ya michezo ya pamoja.
7. Changanua stadi nne zinazohitajika ili kuongeza ufanisi wa mchezaji katika mpira wa mikono.
8. Eleza faida nne za televisheni na redio katika kukuza michezo.
9. Eleza mambo manne ya kuzingatia ili kufanikisha mashindano ya michezo ya shule ya msingi.
10. Changanua njia nne ambazo makocha hutumia mawasiliano na wachezaji uwanjani.

## SEHEMU B (30 Alama)

Jibu maswali mawili katika sehemu hii

11. Eleza kwa hoja tano namna michezo inavyoweza kuchangia mshikamano wa kitaifa.
12. Fafanua hatua tano za kutoa huduma ya kwanza kwa mchezaji aliyeanguka na kupata jeraha la kichwa.
13. Eleza mifumo mitatu ya wachezaji katika mpira wa miguu na mchango wake katika mafanikio ya timu.

## SEHEMU C (30 Alama)

Jibu maswali mawili katika sehemu hii

14. Eleza kanuni sita za usalama zinazopaswa kuzingatiwa ili kupunguza ajali katika michezo ya shule.
15. Tathmini mchango wa teknolojia ya mawasiliano katika kuongeza uwekezaji na ufadhili kwenye michezo.
16. Kwa mifano, eleza nafasi ya michezo ya asili katika kukuza maadili na mshikamano wa kijamii.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org